


# Alichokisema dada yake Vusi

## Vusi



- Nina Orange
  - Wiehan de Jager
  - Matteo E. Mwita
- 4
- 




# Global Storybooks

[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)


## Alichokisema dada yake Vusi

- Nina Orange
- Wiehan de Jager
- Matteo E. Mwita




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.  
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>







Siku moja asubuhi bibi yake Vusi alimwita na kumwambia, "Tafadhali peleka yai hili kwa wazazi wako. Wanataka kutengeneza keki kubwa kwa ajili ya harusi ya dada yako."




Alipokuwa njiani kuelekea kwa wazazi wake, Vusi akakutana na vijana wawili wanaokota matunda. Kijana mmoja akanyakua yai kutoka kwa Vusi na akalirusha kwenye mti. Yai likavunjika.



Dada yake Vusi alifikiria kwa muda, halafu akasema, "Kaka yangu Vusi, usijali zawadi, pia usijali kekii! Tupo hapa pamoja, nina furaha. Nenda kavae nguo zako nadhifu na uje tusherehekee siku hiii!"




“Umefanya nini?” Vusi akalia. “Yai lile lilikuwa kwa ajili ya keki. Keki ilikuwa kwa ajili ya harusi ya dada yangu. Dada yangu atasemaje kama hakutakuwa na keki ya harusi?”




“Nifanye nini?” alilia Vusi. “Ng’ombe aliyekimbia alikuwa ni zawadi, ambayo nilipewa kama mbadala wa makuti niliyopewa na wajenzi. Wajenzi walinipa makuti kwa sababu walivunja fimbo niliyopewa na waangua matunda. Waangua matunda walinipa fimbo kwa sababu walivunja yai la keki. Keki ilikuwa kwa ajili ya harusi. Kwa hiyo hakuna yai, hakuna keki, na hakuna zawadi.”



Vijana wale waliomba msamaha kwa kumchokoza Vusi. "Hatuna la kufanya kuhusu keki, lakini hii hapa ni fimbo kwa ajili ya dada yako," mmoja alisema. Vusi akaendelea na safari yake.




Lakini wakati wa chakula cha jioni ng'ombe alikimbia kurudi kwa mkuimba. Na Vusi akapotea njiani. Akafika kwa kuchelewa sana kwenye harus! ya dada yake. Wageni walikuwa tayari wanakula.




Njiani alikutana na wanaume wawili wakijenga nyumba. “Tunaweza kutumia hiyo fimbo imara?” mmoja akaomba. Lakini fimbo haikuwa imara kwa kujengea, na ikavunjika.




Ng’ombe aliomba msamaha kwa kuwa mlafi. Mkulima alikubali kumpa Vusi ng’ombe aende naye kama zawadi kwa ajili ya dada yake. Vusi akaendelea na safari yake.




“Mmetanya ninini?” Vusi akalia. “Fimbo hii  
ilikuwa zawadi kwa ajili ya dada yangu.  
Waangua matunda waliinipa fimbo hiyo  
kwa sababu waliunja yai la keki. Keki  
ilikuwa ni kwa ajili ya harussi ya dada  
yangu. Sasa hakuna yai, hakuna keki, na  
hakuna zawadi. Dada yangu atasemaje?”



“Umetanya ninini?” Vusi akalia. “Makuti haya  
yalikuwa zawadi ya dada yangu. Wajenzi  
waliinipa makuti kwa kuwa waliunja fimbo  
yangu niliyopewa na waangua matunda.  
Waangua matunda waliinipa fimbo kwa  
kuwa waliunja yai kwa ajili ya keki ya dada  
yangu. Keki ilikuwa kwa ajili ya harussi ya  
dada yangu. Sasa hakuna yai, hakuna keki,  
na hakuna zawadi. Dada yangu  
atasemaje?”



Wajenzi waliomba msamaha kwa kuvunja fimbo. “Hatuna la kufanya kuhusu keki, lakini tutakupa makuti umpelekee dada yako,” mmoja alisema. Na Vusi akaendelea na safari yake.



Njiani, Vusi akakutana na mkulima akiwa na ng’ombe. “Una makuti mazuri, naweza kupata kidogo?” Ng’ombe akaomba. Lakini makuti yalikuwa matamu ng’ombe akayala yote!